KUMBUKUMBU ZA SHUGHULI ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO

MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI ROBO YA NNE MWAKA 2020/2021 ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO ULIOPO MAKAO MAKUU YA MANISPAA LUGURUNI
TAREHE 13 AGOSTI 2021

WAJUMBE WALIOHUDHURIA.

NA	JINA	WADHIFA
1.	Mhe. Jaffary Juma Nyaigesha	Mstahiki Meya na Diwani wa Kata ya Ubungo
2.	Mhe. Mwasha Hassan Siraju	Naibu Meya na Diwani wa Kata ya Msigani
3.	Mhe. Laizer Edward Naigisa	Diwani wa Kata ya Saranga
4.	Mhe. Peter Kiango Ikamba	Diwani wa Kata ya Kibamba
5.	Mhe. Shirima Olivery Quirine	Diwani wa Kata ya Makuburi
6.	Mhe. Kimwanga Bakari Hassan	Diwani wa Kata ya Makurumla
7.	Mhe. Klerruu Joseph Thomas	Diwani wa Kata ya Mabibo
8.	Mhe. Awino Raphael Nyangi	Diwani wa Kata ya Sinza
9.	Mhe. Mvungi Ismail Burhani	Diwani wa Kata ya Kimara
10.	Mhe. Esther Ladislaus Ndoha	Diwani wa Kata ya Goba
11.	Mhe.Yusuph Yenga	Diwani wa Kata ya Mburahati
12.	Mhe. Batalingaya N.Richard	Diwani wa Kata ya Kwembe
13.	Mhe. Malata L.Ismail	Diwani wa Kata ya Mbezi
14.	Mhe. Elga Elisha	Diwani wa Viti Maalum
15.	Mhe. Liberatha Samson Nziliule	Diwani wa Viti Maalum
16.	Mhe. Nuru Dunda Mbezi	Diwani wa Viti Maalum
17.	Mhe. Hawa Abdulrahman Ally	Diwani wa Viti Maalum

KATIBU

1.	Beatrice R.Dominic	Mkurugenzi wa Manispaa

WATAALAM WALIOHUDHURIA

NA	JINA	WADHIFA/CHEO
1.	James Mkumbo	Katibu Tawala wa Wilaya
2.	Kateti S.H	Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi
3.	Tumanini E.Mrango	Mweka Hazina wa Manispaa
4.	Justine E.Massangya	Mhasibu wa Mapato wa Manispaa
5.	Paschal Mtey	Mhasibu

6.	Kissah Mbilla	Mwanasheria wa Manispaa
7.	Fadhili Hussein	Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipangomiji
8.	Yusta Bongole	Kny;Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii
9.	Dr.Peter Nsanya	Mganga Mkuu wa Manispaa
10.	Eng:Charles Masedoya	Mkuu wa Idara ya Ujenzi
11.	Lawi Bernard	Mkuu wa Idara ya Hifadhi ya Mazingira na Udhibiti wa taka ngumu
12.	Happiness P.Mbelle	Mkuu wa Idara ya Kilimo, Ushirika na Umwagiliaji
13.	Marcelina A.Saura	Kny;Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi na Ugavi
14.	Mula F.Mohamed	Mkaguzi wa Ndani wa Manispaa
15.	Abdul Buhetty	Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi
16.	Archie J.Mtambo	Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi
17.	Paul O.Ngunga	Afisa Uchaguzi wa Manispaa
18.	Sophia C.Kayombo	Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA
19.	Joina Nzali	Afisa Uhusiano wa Manispaa
20.	Hilda Shalanda	Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari
21.	Prisca Mjema	Afisa Biashara wa Manispaa
22.	Ritha Nguruwe	Afisa Utamaduni wa Manispaa
23.	Happy G.Mwamakula	Kny;Mratibu wa UKIMWI wa Manispaa
24.	David Mbena	Kny; Mratibu wa TASAF
25.	Lusubilo Mwaisunga	Katibu TSC
26.	Bakari Mwamende	Afisa Utumishi
27.	Agnes Kyando	Afisa Tarafa Magomeni
28.	Beatrice Mbawala	Afisa Tarafa Kibamba
29.	Chikauma Athuman	Auxiliary Police

VIONGOZI NA WAGENI WAALIKWA

NA	JINA	WADHIFA/CHEO
1.	Kheri D.James	Mkuu wa Wilaya Ubungo
2.	Lucas Mgonja	Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya
3.	Sylvesther Yaredi	Katibu wa CCM wa Wilaya
4.	Emmanuel B.Tarimo	Kamanda wa TAKUKURU Wilaya
5.	Stellamatutina Kyamani	Afisa Usalama wa Wilaya
6.	Rehema Webiro	Afisa Usalama

7.	Insp.Alex Dogota	OCD - Magomeni
8.	Nicholaus Lawrence	Ag.OCD Mabwepande
9.	Asist.George G.Chimtembo	Afisa Uhamiaji Wilaya
10.	Insp.Isack Njombe	Afisa Zimamoto Ubungo
11.	SGT. Joseph Kitundu	Jeshi la Akiba - Wilaya
12.	Juliana Simon	Afisa Huduma kwa Wateja - DAWASA
13.	Eng.Emmanuel Mwadumbya	Kutoka TARURA
14.	Ezekiel Mashola	Meneja TANESCO - Ubungo

WAJUMBE AMBAO HAWAKUHUDHURIA

NA	JINA	WADHIFA	
1.	Mhe.Prof.Kitila A.Mkumbo	Mbunge wa Jimbo la Ubungo na Waziri wa viwanda na Biashara	— Kwa taarifa
2.	Mhe.Issa J.Mtemvu	Mbunge wa Jimbo la Kibamba	— Kwa taarifa
3.	Mhe. Mariam Nassoro Kissangi	Mbunge wa Viti Maalum	— Kwa taarifa
4.	Mhe. Eliam Manumbu	Diwani wa Kata ya Manzese	— Kwa taarifa
5.	Mhe. Mary B. Mwamfupe	Diwani wa Viti Maalum	— Kwa taarifa

SEKRETARIETI

NA	JINA	WADHIFA/CHEO
1.	Maurus M.Kayombo	Mwandishi wa Mikutano wa Manispaa
2.	Theresia L.Minja	Mwandishi wa Mikutano wa Manispaa

Agenda zilizowasilishwa tarehe 13/08/2021: -

1. Kufungua Mkutano.
2. Kupitia na kuidhinisha ajenda.
3. Maswali ya papo kwa papo kutoka kwa Wajumbe.
4. Kusoma na kuthibitisha Mihtasari ya Baraza la Madiwani ya tarehe 05/05/2021 na 30/06/2021.
5. Kuthibitisha taarifa na Mihtasari ya Kamati za Kudumu za Halmashauri: -

(a). Taarifa ya Kamati ya Huduma za Uchumi, Afya na Elimu robo ya nne kipindi cha Aprili hadi Juni 2020/2021 pamoja na Muhtasari wa Kikao cha Kamati ya Huduma za Uchumi, Afya na Elimu cha tarehe 22/04/2021.

(b). Taarifa ya Kamati ya Mipangomiji na Mazingira robo ya nne kipindi cha Aprili hadi Juni 2020/2021 pamoja na Muhtasari wa Kikao cha Kamati ya Mipangomiji na Mazingira cha tarehe 23/04/2021.

(c). Taarifa ya Kamati ya Maadili ya robo ya nne kipindi cha Aprili hadi Juni 2020/2021 pamoja na Muhtasari wa Kikao cha Kamati ya Maadili cha tarehe 23/04/2021.

(d). Taarifa ya Kamati ya Kudhibiti UKIMWI robo ya nne kipindi cha Aprili hadi Juni 2020/2021 pamoja na Muhtasari wa Kikao cha Kamati ya kudhibiti UKIMWI cha tarehe 16/04/2021.

(e). Taarifa ya Kamati ya Fedha na Uongozi robo ya nne kipindi cha Aprili hadi Juni 2020/2021 pamoja na Mihtasari ya Vikao vya tarehe 18/06/2021, 28/06/2021, 30/06/2021 na 14/07/2021.

6. Mapendekezo ya Sheria Ndogo.

7. Kufunga Mkutano.

UMC/11/21 Kufungua Mkutano.

Mwenyekiti aliwakaribisha Wajumbe wa Baraza la Madiwani, Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, Mwenyekiti na Katibu wa CCM Wilaya, Watendaji na wanahabari kwenye Mkutano wa kawaida wa kujadili taarifa za robo ya nne mwaka wa fedha 2020/2021.Pia alitoa rai kwa Wajumbe wa Baraza kujitokeza kuchanja chanjo ya Uviko 19 ili kujikinga na janga la corona. Baada ya maelezo hayo alifungua Mkutano saa 6:00 mchana.

UMC/12/21 Kupitia na kuidhinisha ajenda.

Wajumbe walipitia ajenda zilizowasilishwa na kukubali zijadiliwe kama zinavyoonekana katika Muhtasari huu.

UMC/13/21 Maswali ya papo kwa papo kutoka kwa Wajumbe.

Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali mbalimbali yaliyojibiwa na Mkurugenzi wa Manispaa kama ifuatavyo: -

13.1 Mhe.Ismail Mvungi Diwani wa Kata ya Kimara aliipongeza Halmashauri na Serikali kuu wa ujumla kwa ujenzi wa hospitali ya Wilaya katika eneo la Kimara Baruti. Alieleza kuwa eneo hilo lilikuwa la Twiga Chemical na Manispaa ilipewa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali. Ndani ya eneo hilo wapo wananchi walioanza kuishi toka mwaka 1960. Baadhi ya wananchi wana Hati na wengine hawana hati. Je, mpango wa Halmashauri kushughulia wakazi walio ndani ya eneo la hospitali upoje?

Katibu wa Kikao alijibu kwamba ni kweli Serikali kuu kupitia Msajili wa Hazina ilikabidhi eneo la ekari 35 kwa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kwa ajili ya ujenzi wa hospitali. Hata hivyo Halmashauri imeshindwa kupata ekari zote kwa kuwa ndani ya eneo hilo kuna wakazi walioendeleza nyumba za makazi. Hivyo kati ya ekari 35

ambazo Manispaa ilitakiwa kupata, imeweza kupata ekari tano (5) tu. Msajiri wa Hazina anashughulikia taratibu za kufuta Hati ya awali ili Manispaa ipewe Hati yake. Mara baada ya taratibu hizo kukamilika, Viongozi ngazi ya Wilaya, Kata na Mtaa watashirikishwa ili kubaini wanaostahili kuendelea kuwepo katika eneo hilo au kuondolewa kwa makubaliano yatakayoafikiwa na pande zote mbili.

13.2 Mhe.Esther Ndoha Diwani wa Kata ya Goba aliuliza ni jinsi gani Menejimenti imejipanga kudhibiti upotevu wa mapato katika stendi ya mabasi ya Magufuli kwa kuwa yeye mwenyewe aliwahi kutoa fedha getini na hakupewa risiti.

Katibu wa Kikao alikiri kuwa ni kweli changamoto ya upotevu wa mapato katika stendi ya mabasi ya Magufuli ipo. Halmashauri imeandika barua kwenda kwa Katibu Mkuu TAMISEMI kuomba Kituo hicho kufungiwa mfumo wa *ki -eletronic* kwenye mageti ya kuingilia abiria na magari (kama ilivyo kwa daraja la Mwalilmu Nyerere Kigamboni). Hivyo suala hilo linafanyiwa kazi.

13.3 Mhe.Eliga Eisha Mwamkinga Diwani wa Viti maalum aliuliza baada ya bajeti ya Halmashauri ya mwaka 2021/2022 kupitishwa na Baraza la Madiwani hawajapata mrejesho kama Hazina walipitisha au hawakupitisha.

Katibu wa Kikao alijibu kwamba Wahe.Madiwani wote watasambaziwa kwenye Vishkwambi Bajeti ya Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo iliyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

13.4 Mhe.Nura D. Mbezi Diwani wa Viti Maalum aliuliza mpango wa Manispaa kupandisha hadhi zahanati ya Mavurunza kuwa Kituo cha Afya kwani inahudumia wagonjwa wengi ikiwa ni pamoja na wale wanaotokea Manispaa ya Ilala.

Katibu wa Kikao alijibu kwamba Idara ya Afya na ustawi wa Jamii italifanyika kazi suala hilo kulingana na miongozo ya Wizara ya Afya.

13.5 Mhe.Nicholaus Batalingaya Diwani wa Kata ya Kwembe aliomba Halmashauri ijenge Shule ya Msingi na Kituo cha Afya katika Mtaa wa Njeteni kwani lipo eneo la ekari 75 linalotosha kuweka huduma hizo.

Katibu wa Kikao alieleza kwamba Kata ya Kwembe ni moja kati ya Kata zenye zahanati nyingi ikiwemo zahanati ya Kwembe, Amani na na King'azi B. Pia wakazi wa Kwembe wapo karibu na hospitali ya Mlaganzila tofauti na Kata zingine.

13.6. Mhe.Bakari Kimwanga Diwani wa Kata ya Makurumla alieleza kuwa Kituo cha Afya cha Makurumla kinahudumia wagonjwa wengi kutoka Kata tano. Wakati wa rufaa wagonjwa wengi wanapata shida kwa kuwa hakuna gari la wagonjwa. Je, Halmashauri inao mpango gani wa kutoa gari la wagonjwa kwa Kituo cha Afya Makurumla?

Katibu wa Kikao alifafanua kuwa Ambulance iliyopo haitoi huduma kwa Kituo kimoja tu cha afya bali kwa vituo vyote vilivyopo ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo.

Katika bajeti ya mwaka 2021/2022, Halmashauri imejipanga kununua ambulance mbili (2). Aidha ambulance mbovu zitafanyiwa matengnezo ili ziweze kutoa huduma kwa wagonjwa wanaohitaji rufaa.

13.7. Mhe.Ismail Malata Diwani wa Kata ya Mbezi aliuliza kwamba wakati wa Baraza la Mgawanyo wa mali za zilizokuwa za Jiji la Dar es Salaam, Baraza liliazimia Menejimenti ishughulikie kupunguza gharama za kukodi fremu katika stendi ya mabasi ya Magufuli kwa kuwa nyingi hazijapata wapangaji kwa sababu ya gharama kuwa kubwa. Je, hadi sasa suala hilo limefikia wapi?

Katibu wa Kikao alijibu kuwa taarifa juu ya suala hilo iliandikwa na kuwasilishwa TAMISEMI. Hivyo Menejimenti bado inaendelea kufuatilia suala hilo.

13.8 Mhe.Joseph T. Krerruu Diwani wa Kata ya Mabibo alieleza kuwa changamoto kubwa ya Kata ya Mabibo ni kukosekana kwa vivuko 17 (vidogo 3 na vikubwa 14). Changamoto hii imeshindwa kutatuliwa kutokana na kukokekana kwa michoro ya kitalaam ya ujenzi wa vivuko. Kwa mfano katika Mtaa wa Mabibo Tsh.27mil/= zilitumika kujenga kivuko ambacho kilisombwa na maji kwa sababu kulikuwa hakuna michoro ya kitaalamu. Hivyo Wahandisi wafike Kata na kuandaa michoro ya kitaalam ya vivuko pamoja na gharama za ujenzi.

Akifafanua hoja hiyo, Katibu wa Kikao aliwakumbusha Wahe.Madiwani kwamba suala la matengenezo ya barabara, madaraja na vivuko lipo chini ya TARURA. Hata

hivyo Halmashauri itaendelea kushirikiana na TARURA. Kwa kuwa watumishi wa TARURA wamehudhuria Mkutano huu na hoja ya Mhe.Diwani wameisikia, ni vyema TARURA kwa washirikiane na Idara ya Ujenzi kuifanyia kazi hoja ya Mhe.Diwani.

UMC/14/21 Kusoma na kuthibitisha Mihtasari ya Baraza la Madiwani ya tarehe 05/05/2021 na 30/06/2021.

Wajumbe walisoma Mihtasari ya Baraza la Madiwani ya tarehe 05/05/2021 na 30/06/2021 na kupitisha kuwa kumbukumbu sahihi za Halmashauri.

UMC/15/21 Kupokea taarifa za Kamati za kudumu: -

15.1 Taarifa ya Kamati ya Huduma za Uchumi, Afya na Elimu robo ya nne kipindi cha Aprili hadi Juni 2020/2021 pamoja na Muhtasari wa Kikao cha Kamati ya Huduma za Uchumi, Afya na Elimu cha tarehe 22/04/2021.

Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Uchumi, Afya na Elimu aliwasilisha taarifa ya robo ya nne kipindi cha Aprili hadi Juni 2020/2021 pamoja na Muhtasari wa Kikao cha Kamati ya Huduma za Uchumi, Afya na Elimu cha tarehe 22/04/2021. Ilielezwa kuwa Kamati ya Huduma za Uchumi, Afya na Elimu ilifanya Kikao cha robo ya nne tarehe 09/08/2021 na kuazimia mambo mbalimbali yakiwemo yafuatavyo: -

Wahe. Madiwani wapewe mafunzo ya namna ya kutumia Vishkwambi ili kuwezesha Vikao vya Kamati kufanyika kwa ufanisi, Kamati itembelee Hospitali ya Wilaya –Kimara Baruti ili kuona hali halisi ya ujenzi na kushauri ipasavyo, Halmashauri ione umuhimu wa kutumia maeneo yaliyo pembezoni mwa barabara ya TANROAD kama vitega uchumi vya biashara kwa kuweka *temporary structures.* Pia Wajumbe walishauri kuwa atafutwe Mkandarasi mwingine atakayemalizia ujenzi wa zahanati hiyo kwa

kuwa aliyepo amechelewesha kazi, Aidha taarifa ya hali halisi ya mradi huu iwasilishwe kikao kijacho ikifafanua namna ya kutatua changamoto hii. Aidha Idara ya Ujenzi iandae taarifa ya hali halisi ya mradi huo pamoja na changamoto zilizotokea na kuwasilisha kwenye Kikao Kijacho.

Wajumbe walipitisha taarifa hii.

15.2 Taarifa ya Kamati ya Mipangomiji na Mazingiara robo ya nne kipindi cha Aprili – Juni, 2020/2021 pamoja na Muhtasari wa Kikao cha tarehe 23/04/2021.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mipangomiji na Mazingira aliwasilisha taarifa ya kipindi cha robo ya nne Aprili – Juni, 2020/2021 pamoja na Muhtasari wa Kikao cha tarehe 23/04/2021. Pia alieleza kuwa Kamati ya Mipangomiji na Mazingira ilifanya Kikao cha robo ya nne tarehe 09/08/2021 na kuazimia mambo mbalimbali yakiwemo yafuatayo: - Wahe. Madiwani wapewe semina ya namna ya kutumia Vishkwambi, Wataalamu wa Manispaa wafuatilie utekelezaji wa Ilani waliyoitoa katika Kiwanda cha magazeti cha Mwananchi kuhusiana na utiririshaji wa maji machafu. Pia Menejimenti ifanye utaratibu/zoezi la kuwaondoa wamachinga ndani ya kituo cha Mabasi cha Magufuli. Aidha ni vyema mitambo ya kiwanda cha lami ikaguliwe ili kujua uimara wake.

Mhe.Esther L.Ndoha Diwani wa Kata ya Goba aliuliza namna Manispaa ilivyojipanga kudhibiti tatizo la uchimbaji mchanga.

Mkuu wa Idara ya Hifadhi ya Mazingira na Udhibiti wa taka ngumu alieleza kuwa mpaka sasa uchimbaji holela wa

mchanga katika Kata ya Goba umesimamishwa na doria imewekwa. Hata hivyo suala hili linahitaji ushirikiano wa pamoja na ufuatiliaji unaendelea.

Wajumbe walipitisha taarifa hii.

9.14 Taarifa ya Kamati ya Maadili ya nne kipindi cha Aprili hadi Juni 2020/2021 pamoja na Muhtasari wa Kikao cha Kamati ya Maadili cha tarehe 23/04/2021.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili aliwasilisha taarifa robo ya nne kipindi cha Aprili hadi Juni 2020/2021 pamoja na Muhtasari wa Kikao cha Kamati ya Maadili wa tarehe 23/04/2021. Alieleza kuwa hali ya Maadili ya Wahe.Madiwani imeendelea kuwa nzuri. Aidha hali ya umoja na mshikamano katika utendaji kazi miongoni mwa Wahe. Madiwani na Watumishi imekuwa nzuri. Kamati ina-toa wito kwa Wahe. Madiwani kuendeleza umoja na mshikamano ili kuleta ufanisi wa kazi kwenye Halmashauri yetu. Kamati ya Maadili ilifanya Kikao cha robo ya nne tarehe 09/08/2021 na kuazimia kuwa Wahe. Madiwani wapewe semina ya matumizi ya Vishkwambi ili kuepuka kutumia muda mrefu kwenye Vikao.

Wajumbe walipitisha taarifa hii.

9.15 Taarifa ya Kamati ya Kudhibiti UKIMWI robo ya nne kipindi cha Aprili hadi Juni 2020/2021 pamoja na Muhtasari wa Kikao cha Kamati ya kudhibiti UKIMWI ha tarehe 16/04/2021.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudhibiti UKIMWI aliwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudhibiti UKIMWI robo ya nne kipindi cha Aprili hadi Juni 2020/2021 pamoja na Muhtasari wa Kikao cha Kamati ya kudhibiti UKIMWI ha tarehe 16/04/2021. Kamati inasisitiza kuwa mpango kazi wa kutembelea club za UKIMWI mashuleni kwa Kata zote

uendelee, ili kuwahamasisha na kuwapa elimu ya kujiepusha na maambukizi ya VVU. Mpaka sasa shule 28 zimetembelewa.

Wajumbe walipitisha taarifa hii.

9.16 Taarifa ya Kamati ya Fedha na Uongozi robo ya nne kipindi cha Aprili hadi Juni 2020/2021 pamoja na Mihtasari ya Vikao vya tarehe 18/06/2021, 28/06/2021, 30/06/2021 na 14/07/2021.

Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uongozi aliwasilisha taarifa ya Kamati ya Fedha na Uongozi robo ya nne kipindi cha Aprili hadi Juni 2020/2021 pamoja na Mihtasari ya Vikao vya tarehe 18/06/2021, 28/06/2021, 30/06/2021 na 14/07/2021. Pia Mwenyekiti alieleza kuwa Kamati ilitembelea mradi wa ujenzi wa vyumba vya madarasa 2 na choo matundu 12 Shule ya Sekondari Malambamawili, ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika Shule ya Msingi Makamba na ujenzi wa wodi ya wazazi katika Za-hanati ya Goba.

Mapato ya mwaka 2020/ 2021

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo iliidhinishiwa bajeti ya kukusanya, kupokea na kutumia jumla ya Sh. 81,632,679,098. Kati ya fedha hizo Sh. 18,002,948.57 ni mapato ya vyanzo vya ndani, Sh.63,629,730,241 ni ruzuku kutoka Serikali kuu na washirika wa maendeleo, ikijumuisha Sh.53,401,596,822 mishahara, Sh. 3,261,133,496 matumizi mengineyo, Sh 1,895,927,823 fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo Idara ya afya na Sh.5,071,072,100 miradi ya maendeleo. Pia Halmashauri ilianza mwaka 2020/21 ikiwa na fedha za

bakaa Sh.2,753,112,870.17 na kufanya bajeti kuu kufikia jumla ya shs. 84,385,791,968.17. Hadi kufikia mwisho wa robo ya nne, Halmashauri imefanikiwa kukusanya mapato ya ndani yenye jumla ya Sh 18,124,621,017 sawa na 101% ya lengo la mwaka.

Mapato ya Kituo cha Mabasi Magufuli.

Kituo hiki hadi kufikia mwisho wa robo ya nne ya mwaka 2020/2021 kimeweza kukusanya jumla ya Tshs 963,278,125, makusanyo haya yanatokana na mchanganuo ufuatao; Tshs 745,476,550 ni mapato ya vizuizi na maegesho, Tshs. 630,900 ni makusanyo yatokanayo na mapato mengineyo, Tshs. 435,000 ni makusanyo yatokanayo na adhabu, Tshs 71,351,500 ni upangishaji wa maeneo na Tshs.145,384,175 ni makusanyo ya huduma ya vyoo. Aidha hadi kufikia robo ya nne kiasi cha Tshs 254,108,250.00 kimekwisha tumika ikiwa ni gharama za uendeshaji wa kituo hicho.

Matumizi ya robo ya nne mwaka 2020/2021.

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo imekadiria kutumia jumla ya Sh. 81,632,679,098. Aidha kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Halmashauri ilivuka na bakaa ya kiasi cha Sh. 2,753,112,870.17, na hivyo kufanya jumla ya makisio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kuwa Sh. 84,385,791,968.17 Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kwa mwezi Juni 2021 ilitumia jumla ya Sh 17,555,521,774. Kati ya matumizi tajwa, Sh 4,,479,578,939 ilitumika kulipia mishahara ya watumishi sawa na asilimia 93 ya lengo la mwezi, Sh 1,021,757,461 Matumizi ya kawaida ya fedha

za ndani za Halmashauri (Reccurent Own source) na Sh 899,670,495 matumizi ya miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na vyanzo vya ndani (Own Source), Sh 87,952,109 ni matumizi ya kawaida ya ruzuku kutoka serikali kuu (OC), sh.1,026,532,136 ni mishahara ya watumishi inayofadhiliwa na mfuko wa MDH(Management and Development for Health).

Kamati ya Fedha na Uongozi ilifanya Kikao cha robo ya nne tarehe 10/08/2021 na kuazimia mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na yafuatayo: -

Mkuu wa Idara ya Ujenzi afanye tathmini ya gharama za ujenzi zilizotumika katika jengo la ofisi za mapato Simu 2000, kiasi alicholipwa mjenzi, kiasi ambacho hakijalipwa na kutoa ushauri wa namna ya kukamilisha mradi huo, iandaliwe taarifa ya kazi zilizofanywa na Makampuni ya urasimishashaji ndani ya Halmashauri ikionesha makusanyo yaliyokusanywa na matumizi ya fedha hizo. Pia Kamati ya Fedha na Utawala ifanye ziara ya kukagua soko hilo na kufanya mazungumzo na Uongozi wa soko ili kuona namna ya kurudisha mapato ya Manispaa yanayopotea sokoni hapo.

Baada ya kuwasilishwa taarifa hiyo Wajumbe waliuliza maswali kama ifuatavyo:-

Mhe. Ismail Mvungi Diwani wa Kata ya Kimara aliuliza kuhusu kiwanda cha kufyatua tofali kimefikia hatua gani.

Mkuu wa Idara ya Ujenzi alijibu kwamba baada ya wiki tatu taratibu zote za kiwanda kuanza kufanya kazi zitakuwa zimekamilika.

Mhe.Nicholaus Batalingaya Diwani wa Kata ya Kwembe aliuliza hali ya soko la Mabibo.

Katibu wa Kikao alijibu kwamba ufuatiliaji umefanyika kwa Kamishna wa Ardhi na ameleza kuwa eneo hilo lipo chini ya Msajili wa Hazina. Menejimenti inaendelea kufuatilia suala hilo.

Mhe.Thomas Klerruu Diwani wa Kata ya Mabibo aliuliza mpango wa Halmashauri kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara.

Katibu wa Kamati alijibu kwamba pamoja na kwamba kazi ya matengenezo ya barabara ni jukumu la TARURA, hata hivyo Halmashauri imetenga fedha kidogo kwa ajili ya matengenezo ya barabara.

Wajumbe walipitisha taarifa hii.

Nasaha za Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya.

Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya alimpongeza Mkurugenzi kwa kuteuliwa na Mhe.Rais kuendelea kuwa Mkurugenzi katika Manispaa ya Ubungo. Alipongeza Halmashauri katika jitihada za ukusanyaji wa mapato.

Alieleza kuwa DAWASA, TANESCO, TARURA na Mamlaka ya Bonde wanapoalikwa kwenye Vikao wasiwe wasikilizaji tu, bali wapewe fursa ya kuwasiliisha mipango yao.

Nasaha za Mkuu wa Wilaya.

Mkuu wa Wilaya alipongeza Baraza la Madiwani kwa kazi inayofanya ya kujadili hoja kwa masilahi ya wakazi wa

Ubungo. Hivyo maazimio ya Vikao yawe kwa ajili ya kujibu kero za wananchi. Aidha aamuzi yakishapitishwa na Baraza ni lazima yatekelezwe.

Alieleza kuwa tatizo lilipo ni ngazi za chini za watendaji kutokutekeleza wajibu wao ipasavyo. Kuhusiana na hilo aligusia mambo yafuatayo: -

Katika hospitali ya sinza kuna mgonjwa alipokelewa saa 3:00 usiku na hakupewa dawa hadi saa 5:00 usiku.

Maeneo ya wazi (open space) yaliyopo katika Kata yanatumika kibiashara na Watendaji wa Kata hawachukui hatua zozote.

Katika ziara iliyofanyika Kata ya Makuburi - barabara ya Mandela kuna wananchi waliokuwa wanafanya biashara hadi kwenye akiba ya barabara na waliamriwa kuondoka. Jambo la ajabu ni kwamba Mjumbe wa Mtaa akishirikiana na Mtendaji wa Mtaa amewasainisha mika-taba na wamerudi tena kuendelea na biashara zao katika eneo hilo. Hivyo Mtendaji wa Mtaa huo aondolewa na taratibu za utumishi zifuatwe.

Katika Mtaa wa Kisiwani wananchi wameazimia kujenga ofisi ya Mtaa. Mwenyekiti wa Mtaa anaunga mkono wazo hilo lakini Mtendaji wa Mtaa haungi mkono kwa madai kwamba si kipaumbele cha Halmashauri.

Katika shule ya Msingi Msingwa kuna eneo linalohitaji kusawazishwa ili litumike kama kiwanja cha michezo lakini suala hilo linachukua muda mrefu.

Wawakilishi wa DAWASA, TARURA na TANESCO wanapoalikwa kwenye vikao wawe wanapewa nafasi ya kujibu hoja za Wajumbe.

UMC/10/21 **<u>Kufunga Mkutano.</u>**

Mwenyekiti aliwashukuru Wajumbe, Wageni waalikwa na vyombo vya habari kwa uvumilivu mkubwa walioonesha. toka mwanzo wa kikao hadi mwisho. Pia alihamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi kuchanja chanjo ya uviko 19. Baada ya maelezo hayo alifunga Mkutano saa 11:20 jioni.

UMETHIBITISHWA

_____ _____

MWENYEKITI **KATIBU**

TAREHE _____